

TPDC

JARIDA LA DESEMBA, 2024

SHIRIKA LA
MAENDELEO
YA PETROLI
TANZANIA



TOLEO LA 24

www.tpdcc.co.tz



tpdcc.tz

TPDC YATOA UFAFANUZI CHANGAMOTO YA VITUO VYA KUJAZIA GESI ASILIA KWENYE MAGARI

Uk. 12

***TPDC Takes Action to Overcome Challenges
in Accessing Natural Gas Filling Stations for
Vehicles***

Page. 27

YALIYOMO

- KADHIA YA KUJAZA GESI ASILIA KWENYE MAGARI KUTATULIWA HIVI KARIBUNI
- MIRADI YA GESI ASILIA KUWANUFAISHA WANANCHI
- MWENYEKITI WA BODI YA WAKURUGENZI TPDC ASHIRIKI KONGAMANO LA INDONESIA AFRIKA
- TIMU YA TPDC SHIMMUTA TANGA 2024 YAWAKUMBUKA WAHITAJI KWA KUTOA MISAADA KITUO CHA WATOTO YATIMA
- TPDC MDHAMINI MKUU MBIO ZA MWL. NYERERE MARATHON
- TPDC YACHANGIA SHILINGI MILIONI 50 JKCI
- UCHUKUAJI TAARIFA ZA UTAFITI ENEO LA NCHI KAVU BONDE LA EYASI WEMBERE, WAKAMILIKA
- TPDC YAPONGEZWA UHAMASISHAJI WA MATUMIZI YA NISHATI SAFI
- TPDC YATOA UFAFANUZI CHANGAMOTO YA VITUO VYA KUJAZIA GESI ASILIA KWENYE MAGARI
- UJENZI WA MRADI WA EACOP WAFIKIA ASILIMIA 45.5
- TPDC YAPONGEZWA KASI YA UTAFITI WA MAFUTA NA GESI BONDE LA EYASI WEMBERE

CONTENTS

- NATURAL GAS FILLING STATION CHALLENGES TO BE RESOLVED RECENTLY
- DEPUTY MINISTER HON. JUDITH KAPINGA PRAISES PRESIDENT SAMIA SULUHU HASSAN'S FOCUS ON COMMUNITY DEVELOPMENT
- CHAIRMAN OF THE BOARD OF DIRECTORS TPDC ATTENDS THE CONFERENCE OF INDONESIA AFRICA
- TPDC SHIMMUTA TANGA 2024 TEAM UPLIFTS COMMUNITY WITH GENEROUS DONATION TO ORPHANAGE
- TPDC MAIN SPONSOR MWL. NYERERE MARATHON
- TPDC DONATES 50 MILLION SHILLINGS TO SUPPORT CHILDREN'S HEART TREATMENT AT JKCI COLLECTION OF RESEARCH INFORMATION DRY LAND EYASI WEMBERE VALLEY COMPLETED
- ZANZIBAR ENERGY MINISTER APPLAUDS TPDC'S EFFORTS IN ADVANCING CLEAN ENERGY
- TPDC TAKES ACTION TO OVERCOME CHALLENGES IN ACCESSING NATURAL GAS FILLING STATIONS FOR VEHICLES
- EACOP CONSTRUCTION HITS 45.5% MILESTONE, DRIVING SOCIO-ECONOMIC GROWTH
- TPDC'S EYASI WEMBERE OIL AND GAS EXPLORATION PROJECT REACHES 40% COMPLETION





Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania

TAHARIRI

Ndugu msomaji wa jarida hili maalum la TPDC linalolenga kukupa taarifa za utekelezaji wa majukumu kadha wa kadha ya Shirika, mafanikio, changamoto na namna ambavyo tunavyoweka jitihada za kutatua changamoto na kuhakikisha taifa linanufaika na uwepo wetu, karibu katika toleo hili uweze kujifunza na kuelewa mengi kuhusu TPDC.

Kwanza kabisa tunayofuraha kukuweka wazi ili uweze kuelewa TPDC ni nini hasa katika uchumi wa nchi.

Sisi kama Shirika lolote la Umma tunawajibu kwa mujibu wa sheria kutekeleza yale majukumu ambayo yapo katika sheria za mashirika ya umma lakini pia sheria ya Mafuta ya mwaka 2015 na jukumu letu kubwa zaidi ni kuhakikisha tunatengeneza faida ili kuwaletea wananchi maendeleo kutokana na kazi zetu lakini kuhakikisha kuwa Serikali inaingiza mapato kupitia shughuli zetu.

Sisi TPDC tunajiona kama mhimili muhimu wa maendeleo ya taifa na hii ni kwasababu kutokana na shughuli zetu za utafutaji wa mafuta na gesi asilia, usafirishaji, usambazaji wa gesi asilia nchini tumekuwa ndio watoaji wakuu wa nishati na chanzo cha nishati ya umeme kupitia gesi asilia nchini.

TPDC toka mwaka 2015 hadi leo tunajivunia kuendelea kuwa kichocheo kikuu cha ukuaji wa uwekezaji wa viwanda vikubwa nchini kupitia upatikanaji wa nishati ya uhakika ya gesi asilia kwa mahitaji ya uendeshaji wa viwanda nchini.

Tunatambua kuwa sekta binafsi na haswa viwanda ndio mwajiri mkuu, mlipa kodi mkuu na vina chochea kwa kiasi kikubwa ukuaji wa sekta nyingine kama madini, kilimo, ufugaji, afya, elimu na kadhalika. Hivyo sisi TPDC tumejidhatiti kuhakikisha Tanzania inakua na nishati ya uhakika, yakutosha na nafuu kwa wawekezaji kuwekeza nchini.

Pamoja na kuwepo na miundombinu ya kuchakata gesi asilia Madimba Mtwara na Songo Songo Lindi pamoja na bomba lenye uwezo mkubwa wa kusafirisha gesi pamoja na ujuzi wa ujenzi wa miundombinu ya kusambaza na kuunganisha wateja, TPDC imejikita kwenye miradi ya uongezaji wa gesi asilia nchini ili kuweza kutosheleza mahitaji ya ndani na nje ya nchi.

Kama anavyoeleza Mkurugenzi Mtendaji wa TPDC ndugu Mussa Makame kuwa TPDC kwa sasa kwa kushirikiana na wawekezaji ambao ni ARA Petroleum na Ndovu Resources kupitia gesi iliyogunduliwa Ntorya wataongeza kiasi cha gesi asilia futi za ujazo milioni 60 kwa kuanzia na hadi kufikia 140 katika kipindi cha miaka mitatu pamoja na kuweka mitambo ya kuongeza uwezo wa kuzalisha gesi asilia wa visima vya kitalu cha Mnazi Bay ambapo kiasi cha futi za ujazo milioni 20 za gesi asilia kinatarajiwa kuongezwa.

Aidha TPDC na M&P wanatarajiwa kuchimba visima viwili zaidi katika kitalu hicho cha Mnazi Bay ili kulihakikishia taifa gesi ya kutosha hii ni pamoja na kuendelea na utafiti katika maeneo mengine nchini pamoja na kuingia mikataba yenye tija ya uwekezaji katika sekta ya mafuta na gesi nchini.

Akilihakikishia taifa utashi mwema wa Shirika kwenye kuliletea maendeleo taifa Mussa Makame anasema “TPDC ina jukumu kubwa la kulinda maslahi ya Taifa katika sekta na kumiliki hisa katika vitalu vya uendelezaji na uendeshaji katika vitalu vya mafuta na gesi kwa hiyo utiaji saina kwenye mikataba hii ni hatua kubwa kwa TPDC na ya kihistoria kwa taifa letu kwa kampuni ya Taifa ya Mafuta na Gesi kuweza kununua hisa na kuwa sehemu ya umiliki mkubwa katika kitalu cha Mnazibay”.

TPDC pamoja na kuonyesha uwezo wa kitaalam na kifedha wa kununua hisa katika kitalu cha Mnazi Bay kwa kiasi cha shilingi bilioni 60, shirika limeendela na miradi mingine ikiwemo ile ya utafiti wa mafuta katika kitalu cha Eyasi Wembere pamoja na kuunganisha gesi asilia viwanda na watumiaji wa viwandani na kwenye Taasisi.

Tutaendelea kulihakikishia taifa uwepo wa nishati ya kwetu ya uhakika pamoja na kuliletea taifa maendeleo kwa kuendelea na uwekezaji ndani na hata nje ya nchi.

#TPDCtunawezeshaMaisha!





KADHIA YA KUJAZA GESI ASILIA KWENYE MAGARI KUTATULIWA HIVI KARIBUNI

Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati Mhandisi Felichesmi Mramba amewahakikishia watumiaji wa gesi asilia kwenye magari kuwa kadhia waliokuwa wakiipata kutokana na uhaba wa vituo vya kupata huduma hiyo itafikia ukomo hivi karibuni.

Hayo yalisemwa tarehe 20.09.2024 wakati wa ziara fupi ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa Kituo Mama cha Kushindilia gesi asilia (CNG Mother Station) kinachojengwa na kumilikiwa na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) katika eneo la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam pembezoni mwa barabara ya Sam Nujoma.

“Kwa muda mrefu jijini Dar es Salaam tumekuwa na Kituo kimoja cha Ubungo Maziwa kikifuatiwa na kile cha Tazara na cha sasa hivi Kituo cha tatu ni kile cha Uwanja wa Ndege lakini kituo kinachojengwa hapa kitakuwa kikubwa zaidi kuliko vilivyopo kwa sasa kwahiyo uwepo na kukamilika kwa Kituo hiki mwishoni mwa mwaka hivi kwenye vituo

vilivyopo sasa hazitokuwepo” ameeleza Mha. Mramba.

“Kwanza naomba nitoe rai kwa watanzania wanavyoona Serikali inafanya uwekezaji mkubwa kama mnavyoona hapa nadhani ni wakati muafaka kwa watu mbalimbali na wenyewe kuwa tayari kubadilisha magari yao ili yaweze kutumia gesi asilia.”

Akielezea huduma zitakazotolewa na Kituo hicho Mha. Mramba alibainisha kuwa Kituo kitakua na eneo la kujaza gesi kwenye magari makubwa ya kusambaza gesi asilia pamoja na vituo vya kuhamishika, kujaza gesi kwenye magari yanayotumia gesi asilia na kutakua na karakana ya kuweka mifumo ya gesi asilia kwenye magari.

Mha. Mramba amewasisitiza Wananchi kuchangamkia fursa hiyo kwasababu imethibitika kitaalam kabisa ya kwamba ukitumia gesi asilia unaokoa zaidi ya 50% ya gharama ya mafuta, kwa mfano kwa mwezi gari yako inatumia shilingi laki mbili basi kwa

kutumia gesi asilia utatumia chini ya shilingi laki moja. Aidha, kwa upande wake Mha. Mwikwabe Mhono kutoka TPDC ameeleza kuwa mradi umegawanyika katika sehemu kuu mbili ambazo ni kazi za ujenzi na kazi za uundwaji wa mitambo ambapo kwa upande wa kazi za ujenzi amebainisha kuwa zilianza mwishoni mwa mwezi wa sita na hadi sasa tayari ukamilifu wake umefikia 57% na kwa upande wa uundwaji wa mitambo ambao unafanyika nchini China tayari umefikia 99%.

Mradi wa ujenzi wa Kituo Mama cha CNG cha TPDC unaenda sambamba na ujenzi wa vituo vidogo vya hospitali ya Muhimbili na Kiwanda cha Madawa cha Kairuki kilichopo Kibaha.

Kukamilika kwa mradi huu kutawezesha ukuaji wa matumizi ya gesi asilia nchini hata kwenye maeneo ambayo hayajafikiwa na bomba la gesi asilia.



MIRADI YA GESI ASILIA KUWANUFAISHA WANANCHI



Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Judith Kapinga amesema kuwa dhamira ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ni kuhakikisha Wananchi wananufaika na miradi ya maendeleo inayotekelezwa kwenye maeneo yao.

Mhe. Kapinga aliyasema hayo mkoani Mtwara wakati wa ziara ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini iliyolenga kukagua visima vya

kuzalisha gesi asilia katika eneo la Mnazi Bay pamoja na miradi inayofanyika kwa manufaa ya jamii (CSR) kutokana na uwepo wa gesi hiyo ikiwemo ujenzi wa Kituo cha Afya na Kituo cha Polisi katika eneo la Msimbati.

“Yote haya mnayoyaona ni matunda ya kazi nzuri ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye anaonesha kwa vitendo jinsi anavyowajali

kwa kuhakikikisha mnapata huduma bora kupitia miradi hii,” alisema Mhe. Kapinga

Alieleza kuwa lengo la ziara hiyo ya Kamati ya Bunge ni kujionea thamani ya miradi hiyo ambayo itanufaisha Wananchi wa Msimbati, ikiwa ni utekelezaji wa maagizo ya Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko aliyoyatoa mara baada ya kutembelea eneo hilo na kuzungumza na Wananchi.



MWENYEKITI WA BODI YA WAKURUGENZI TPDC ASHIRIKI KONGAMANO LA INDONESIA AFRIKA

Kwa mwaliko wa Serikali ya Indonesia, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) Mhe. Balozi Ombeni Sefue, alihudhuria Kongamano la Indonesia-Afrika mjini Bali

Indonesia.

Pamoja na kushiriki katika mjadala na Viongozi wengine, Balozi Sefue pia alishiriki katika hafla ya makabidhiano ya Hati ya Makubaliano (MOU) kati ya TPDC na

PERTAMINA inayoongeza muda wa ushirikiano kati ya Kampuni hizo mbili kuendelea kushirikiana katika kujenga uwezo pamoja na kutafuta fursa za uwekezaji nchini ya Tanzania.



The 2nd Indonesia - Africa Forum

Bandung Spirit for Africa's Agenda 2063

1-3 SEPTEMBER
2024
BALI, INDONESIA



TIMU YA TPDC SHIMMUTA TANGA 2024 YAWAKUMBUKA WAHITAJI KWA KUTOA MISAADA KITUO CHA WATOTO YATIMA



Timu ya Shirika la Maendeleo ya Petrol Tanzania (TPDC) imeonyesha mfano wa kuigwa kwa kujumuisha juhudi za kusaidia wahitaji katika jamii. Timu hiyo, inayojivunia umahiri ndani na nje ya uwanja, imetekeleza mpango wa kuwasaidia watu wenye uhitaji katika Jiji la Tanga wakati wakishiriki mashindano ya SHIMMUTA TANGA 2024. Kitendo hicho cha kuchangia jamii kimeonesha dhamira ya Shirika kuimarisha maendeleo endelevu kwa vitendo.

Kupitia programu ya Uwajibikaji wa Shirika kwa jamii (CSR), Wachezaji na Viongozi wa timu hiyo walitoa msaada wa vifaa muhimu kwa watoto wanaoishi katika mazingira magumu wanaolelewa katika Kituo cha “Nyumba ya Furaha” kilichopo Tanga Mjini. Timu

ya TPDC ilifanikiwa kutoa vifaa mbalimbali vikiwemo madaftari, unga wa ugali, unga wa ngano, sabuni, mafuta ya kupikia pamoja na fedha taslimu kiasi cha shilingi 300,000 ikiwa ni mchango wa ada kwa mtoto mmoja anaetarajiwa kujiunga na kidato cha kwanza 2025.

Akizungumza baada ya zoezi hilo, Mhandisi Magori Matiku (Makamu Mwenyekiti wa Timu TPDC) alisema kuwa, “Michezo ni zaidi ya ushindani na ni fursa ya kushirikiana na jamii na kuhakikisha tunaleta mabadiliko ya kweli. Timu yetu haiko hapa tu kwa ajili ya kushindana, bali pia kuonyesha mshikamano na jamii inayotuzunguka.”

Hatua hiyo imelenga kuonyesha mshikamano na jamii wanazozihudumia, huku ikilenga kuacha athari chanya ya kudumu.

Aidha, akizungumza kwa niaba ya Kituo hicho, Sister Mlezi Irene Kapuka, aliipongeza TPDC na kushukuru kwa vifaa vilivyotolewa. “Tunawashukuru sana kwa moyo wa upendo mliotuonesha,” alisema Sister Kapuka.

Michezo hii inatajwa kuimarisha mshikamano miongoni mwa Wafanyakazi wa Mashirika mbalimbali nchini, huku yakionyesha namna michezo inaweza kuwa chachu ya maendeleo ya kijamii.

Mashindano ya SHIMMUTA TANGA 2024 yalihitimishwa rasmi tarehe 24.11.2024 ambapo TPDC iliibuka na ushindi wa pili kuvuta kamba kwa upande wa Wanawake na mshindi wa pili pooltable kwa upande wa Wanawake na mshindi wa pili mchezo wa bao kwa upande wa Wanawake.



MBIO ZA HISANI MWANZA

2024



TPDC MDHAMINI MKUU MBIO ZA MWL. NYERERE MARATHON

Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) limekuwa Mdhamini Mkuu wa Mbio za Mwl. Nyerere Marathon zilizofanyika Oktoba 12, 2024 Igoma Mkoani Mwanza. Mbio hizo zimefanyika zikiwa na lengo la kuenzi falsafa ya Hayati Mwalimu Julius Kambarage

Nyerere katika Maendeleo na Ustawi wa Taifa letu.

Akiongea katika hafla hiyo Bw. Donald Aponde ambaye ni Mwakilishi wa Mkurugenzi Mtendaji wa TPDC ameeleza kuwa, "TPDC inajivunia kudhamini mbio hizi kwani

Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alifanya mambo mengi ikiwemo kuanzishwa kwa TPDC (1969) ambapo hadi sasa Shirika letu linafanya vizuri kwenye shuguli za utafutaji na uendelezaji wa nishati ya mafuta na gesi asilia nchini.

TPDC YACHANGIA SHILINGI MILIONI 50 JKCI

Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) limechangia kiasi cha shilingi milioni 50 kwa Taasisi ya moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) kwa lengo la kusaidia watoto wenye uhitaji wa Matibabu ya moyo.

TPDC ilichangia fedha hizo kwenye hafla ya uchangishaji fedha kwaajili ya kusaidia watoto 1500 wenye matatizo ya moyo.

Hafla hiyo ilihudhuriwa na Rais Mstaafu wa awamu ya nne Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete ambaye ndio alikuwa mgeni rasmi.

Tukio hilo lilifanyika tarehe 02.11.2024, Johari Rotana Jijini Dar es salaam.





UCHUKUAJI TAARIFA ZA UTAFITI ENEO LA NCHI KAVU BONDE LA EYASI WEMBERE, WAKAMILIKA

Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) limekamilisha uchukuaaji wa taarifa za utafiti wa mafuta na gesi asilia eneo la nchi kavu katika bonde la Eyasi Wembere lililopo Kaskazini-Mashariki mwa Tanzania kwenye mikoa mitano ya Tabora, Singida, Arusha, Simiyu na Shinyanga ambapo kwa awamu hii, utafiti umegusa mikoa mitatu ambayo ni Singida (Mkalama na Iramba), Simiyu (Meatu) na Arusha (Karatu).

Hayo yalielezwa Novemba, 2024 na Meneja mradi wa utafiti wa mafuta katika Bonde la Eyasi Wembere Mjiofizikia Mwandamizi Sindi Maduhu katika kambi ya utafiti wa mafuta iliyopo Kijiji cha Bukundi Wilayani Meatu ambapo alieleza kuwa awamu hii ya utafiti ilianza mwezi Agosti mwaka huu na hadi sasa

maendeleo ni mazuri kwani taarifa za mitetemo za mfumo wa 2D (2DSeismic Survey) zenye urefu wa kilomita 430 zimekusanywa.

Aidha, Sindi alifafanua kuwa, shughuli za utafiti kwa awamu hii zimegusa mikoa 3 ya Singida Arusha na Simiyu na zilikwenda sambamba na zoezi la uthamini ambapo jumla ya vijiji 15 vya mikoa hiyo vyenye idadi ya waathirika wa mradi 541 wako mbioni kulipwa fidia ya mazao yaliyoharibiwa wakati wa zoezi la utafiti.

Katika hatua nyingine, Sindi amewaeleza Wananchi kuendelea na shughuli zao za maendeleo zikiwemo za kiuchumi kama kilimo, uvuvi, ufugaji na shughuli zingine za kijamii kwani kwa awamu hii shughuli za utafiti zimesitishwa kwa muda na zitaendelea eneo

la majini katika Ziwa Eyasi mwezi Mei, 2025.

Pia, Sindi alishukuru na kupongeza juhudi zinazofanywa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuunga mkono juhudi za utafiti wa mafuta na gesi asilia nchini ikiwemo Bonde la Eyasi Wembere, aidha ameishukuru Wizara ya Nishati, Bodi ya Wakurugenzi na Menejimenti ya TPDC kwa juhudi kubwa za usimamizi na maelekezo ambayo wanayatoa ili kuhakikisha shughuli za utafiti zinakamilika kwa tija na kwa wakati.

Aidha, TPDC na Mkandarasi (AGS) wanaendelea na zoezi la kurejesha mazingira ambayo yaliathiriwa na shughuli za mradi kuwa katika hali yake ya awali (restoration).



TPDC YAPONGEZWA UHAMASISHAJI WA MATUMIZI YA NISHATI SAFI

Waziri wa Maji, Nishati na Madini Serikali ya Mapinduzi Zanzibar Mhe. Shaib Kaduara amepongeza juhudi za Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) katika jitihada za kumuunga mkono Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kuhamasisha matumizi ya nishati safi nchini.

Waziri Kaduara aliyasema hayo alipotembelea banda la Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) katika Kongamano la kumi la jotoardhi Barani Afrika (ARGeo-C10) mnamo tarehe 25.10.2024

katika Kituo cha mikutano cha Kimataifa cha Mwalimu Julius Nyerere JNICC Jijini Dar es salaam.

Akizungumza alipotembelea banda la TPDC Mhe. Kaduara alisema, “naipongeza TPDC kwa kuendelea kuunga mkono jitihada za Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kuhamasisha matumizi ya nishati safi kwa Wanachi mbalimbali nchini.”

Akielezea Mjiofizikia Mwandamizi kutoka TPDC Bw. Gaston Canuty alisema lengo la TPDC kushiriki katika Kongamano hilo ni kuendelea kutoa elimu ya matumizi ya

nishati safi ili iweze kuwafikia Wananchi wengi zaidi.

“TPDC kama Shirika la mafuta la Taifa tunaunga mkono juhudi hizo kwa kufanya utafiti wa mafuta na gesi, kusambaza gesi asilia kwa matumizi ya kuzalisha umeme, matumizi ya viwandani na nishati safi ya kupikia majumbani,” alisema Canuty.

Aidha, Canuty alisema, utafiti na uendelezaji wa mafuta na gesi unaotekelezwa na TPDC utatumika kama daraja la kujenga miundombinu ya kuendeleza nishati Jadidifu.





TPDC YATOA UFAFANUZI CHANGAMOTO YA VITUO VYA KUJAZIA GESI ASILIA KWENYE MAGARI

Dar es salaam,

Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) limetoa ufafanuzi kuhusu changamoto ya upatikanaji wa huduma ya kujaza gesi kwenye magari katika vituo vya kujazia gesi asilia.

Ufafanuzi huo umetolewa na Kaimu Mkurugenzi wa Biashara ya Mafuta na Gesi -TPDC Mhandisi Emmanuel Gilbert wakati akifanya mkutano na Waandishi wa Habari tarehe 03.10.2024 Jijini Dar es salaam.

Mha. Gilbert alisema, changamoto ya upatikanaji wa gesi asilia kwenye magari inatokana na mapokeo ya matumizi ya gesi asilia kwenye magari kuongezeka na hivyo

kusababisha changamoto ya upatikanaji wa huduma ya kujaza gesi kwenye vituo vya kujazia gesi.

Akieleza mikakati ya TPDC katika kutatua changamoto ya vituo amesema, Kituo kinachojengwa na TPDC eneo la Chuo Kikuu Dar es salaam ambacho kitakamilika mwezi Desemba, 2024 kitakuwa na pampu nne za kujaza gesi, na kila pampu itakuwa na nozeli mbili hivyo kutakuwa na nozeli nane zenye uwezo wa kujaza CNG kwenye magari nane kwa wakati mmoja ambapo kwa siku kitajaza zaidi ya magari 2000 na kitakuwa na uwezo wa kushindilia na kujaza gesi (CNG) kwenye malori matatu (CNG tube trailers) kwa wakati

mmoja sawa na malori 24 kwa siku yatakayosafirisha na kusambaza gesi kwenye maeneo mbalimbali.

Aidha, TPDC kwa kushirikiana na Sekta binafsi ipo katika mkakati wa kukamilisha ujenzi wa vituo 13 vya kujaza gesi asilia kwenye magari ifikapo mwezi Julai, 2025.

Katika hatua nyingine Mha. Gilbert alisema kuwa, Kampuni mbalimbali zinaendelea kujitokeza kujenga vituo vya gesi ikiwemo Kampuni ya Mafuta ya PUMA ambayo itaanza ujenzi wa vituo viwili eneo la Mbezi beach na Tegeta Jijini Dar es salaam.





UJENZI WA MRADI WA EACOP WAFIKIA ASILIMIA 45.5

Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), unaunganisha bomba la mafuta ghafi kutoka Hoima nchini Uganda hadi Chongoleani, Tanga, umefikia asilimia 45.5 katika hatua ya ujenzi ambapo shughuli za ujenzi zinaendelea katika maeneo mbalimbali kuanzia Mtukula Kagera mpaka Chongoleani Tanga.

Taarifa hii ilitolewa Oktoba 18, 2024, na Mratibu wa Mradi wa EACOP kutoka Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Bw. Asiadi Mrutu, wakati Wajumbe wa Tume ya Kitaifa ya Mipango ikiwa imeambatana na Bodi ya Wakurugenzi ya TPDC na Menejimenti ya TPDC ilipotembelea eneo la ujenzi wa Kiwanda cha kuweka mifumo ya kupasha na kutunza joto kwenye mabomba katika Kijiji cha Sojo, wilayani Nzega, mkoani Tabora.

Mrutu alisema kufuatia jitihada za Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri

ya Muungano wa Tanzania, utekelezaji wa mradi huu kwa ujumla umefikia asilimia 45.5 ambapo shughuli za ujenzi zinaendelea katika maeneo mbalimbali kuanzia Mtukula Kagera mpaka Chongoleani Tanga na kwamba mpaka kufikia Oktoba 2024 Serikali kupitia TPDC imechangia mtaji wa takribani Shilingi Bilioni 977.6 kwenda kwenye Kampuni ya Mradi EACOP.

“Kiwanda hiki kinaendelea na uzalishaji wa mabomba ambapo mpaka sasa jumla ya mabomba yenye urefu wa kilomita 70.7 yamewekwa mifumo ya kupasha na kutunza joto. Ujenzi wa bomba na miundombinu yake unaendelea,” amesema Mrutu.

Mpaka sasa mradi umeleta mafanikio makubwa ikiwemo fursa za ajira 7,584, manunuzi ya huduma na bidhaa za ndani ya nchi zenye thamani ya takribani Shilingi Bilioni 833.7, mapato kwa Serikali takribani Shilingi Bilioni 40, uhaulishaji wa teknolojia toka kwa Wakandarasi,” alieleza

Mrutu.

Alieleza kuwa ujenzi wa Kiwanda cha kuweka mifumo ya kupasha na kutunza joto kwenye mabomba uliopo Kijiji cha Sojo Wilaya ya Nzega Mkoa wa Tabora umefikia asilimia 93 na ulizinduliwa rasmi na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Doto Biteko mnamo Machi 26, 2024.

“Pamoja na kuwa mwanahisa, TPDC inamiliki ardhi ya mkuza wa bomba na maeneo ya ujenzi wa makambi ambapo mpaka sasa tumefanikiwa kulipa fidia jumla ya shilingi Bilioni 35.1 kwa Wananchi 9,858 kati ya 9,927 sawa na 99.3%. Vilevile mradi umefanikiwa kujenga nyumba 340 za makazi mbadala kwa Wananchi 294 waliopoteza makazi kwenye maeneo ya mradi. Serikali inaendelea kushirikiana na Wanhisa wengine ili kuhakikisha fedha za mradi zinapatikana kwa wakati na utekelezaji unaendelea ili kufikia malengo. Ujenzi unatarajia kukamilika katikati mwa mwaka 2026,” ameongeza Mrutu.





TPDC YAPONGEZWA KASI YA UTAFITI WA MAFUTA NA GESI BONDE LA EYASI WEMBERE

Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) limesema kuwa mradi wa utafiti wa mafuta na gesi kwenye Bonde la Eyasi Wembere lililopo katika mikoa ya Simiyu, Singida na Arusha, Tabora na Shinyanga utekelezaji wake umefikia asilimia 40.

Hayo yalielezwa na Bodi ya Wakurugenzi ya TPDC walipotembelea eneo la mradi wa utafiti wa mafuta na gesi katika Bonde la Eyasi Wembere na kuridhishwa na juhudi zinazofanywa na Shirika hilo.

“Tumejionea kazi nzuri ya utafiti wa mafuta na gesi asilia, na tunaipongeza Menejimenti ya TPDC kwa kusimamia vyema utekelezaji wa utafiti wa mafuta katika Bonde hili kwani hatua iliyofikiwa sasa inaridhisha, pia tunaishukuru Wizara ya Nishati inayoongozwa na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Doto Biteko kwa kuendelea kuunga mkono na kusimamia vizuri shughuli za Bodi,” alisema Balozi Kalaghe ambaye ni Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi.

Mradi huo unaotekelezwa kwa fedha za Serikali kiasi cha shilingi Bilioni 43 ulianza mwaka 2015 ambapo shughuli zinazoendelea kufanyika ni uchukuaji wa taarifa (Data) za mitetemo na kuzichakata ili kupata uhakika wa uwepo wa mafuta au gesi.

Katika hatua nyingine, Mwakilishi wa Mkurugenzi Mtendaji wa TPDC kwenye ziara hiyo, Mkurugenzi wa Mipango na Uwekezaji Bw. Derick Moshi alieleza kuwa mradi wa Eyasi Wembere ni wa kimkakati katika nchi na jukumu la TPDC ni kusimamia shughuli zikamilike kwa wakati.

Naye, Kaimu Meneja wa Utafutaji kutoka TPDC Bw. Simoni Nyalusi alisema kuwa shughuli za utafiti zinazofanyika katika Bonde hilo, zinatekelezwa kwenye maeneo mawili ambayo ni eneo la nchi kavu na eneo la majini ndani ya Ziwa Eyasi.

Alisema kuwa katika eneo la nchi kavu wamefanikiwa

kufikia asilimia 40 ya utafiti huo, ambapo alibainisha kuanza kuonekana kwa viashiria mbalimbali ambavyo vimetoa matumaini makubwa ya uwepo wa mafuta na gesi.

Aidha, Wananchi wanaoishi kwenye Vijiji vinavyoguswa na shughuli za utafiti kwenye mikoa iliyopitiwa na mradi wamekua na matumaini ya matokeo chanya ya mradi huo kwani tayari wameanza kuona faida za moja kwa moja ikiwemo kupata fursa za ajira.

Mkazi wa Kijiji cha Nyahaa Kitongoji cha Ulianzobhe Wilaya ya Mkalama Bw. Njibu Tinha, alieleza kuwa, vijana wengi wamepata ajira kwenye shughuli za mradi ikiwemo ulinzi, mafundi umeme, udereva pamoja na shughuli za ujenzi.

“Mradi huu ni faraja kubwa kwetu sisi Wanachi, tutaendelea kutoa ushirikiano kwa Wataalamu wanaohusika na mradi ili shughuli za utafiti zisikwame,” alisema Njibu.



HABARI PICHA



Naibu Waziri wa Nishati Mhe. Judith Kapinga akiwa katika picha ya pamoja na Menejimenti ya Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) baada ya kikao kazi kilichofanyika Septemba, 2024 Jijini Mwanza



Mkuu wa Mkoa wa Mtwara Mhe. Kanali Patrick Sawala akiwa na Watalam kutoka TPDC walipotembelea ofisini kwake kwa lengo la kutoa taarifa ya utoaji elimu kwa Wateja wanaotumia gesi asilia majumbali mkoani Mtwara





Naibu Waziri wa Nishati Mhe. Judith Kapinga akiwa katika banda la TPDC kwenye Kongamano la 10 la Jotoardhi Barani Afrika (ARGeo-C10) lililofanyika katika Kituo cha mikutano cha Kimataifa cha Mwl. Julius Nyerere (JNICC) Oktoba, 2024 Jijini Dar es salaam



Meneja Mradi wa utafutaji wa mafuta na gesi katika Kitalu cha Eyasi Wembere Mjiofizikia Mwandamizi Sindi Maduhu akitoa elimu kwa Wanafunzi wa Shule ya Msingi Mwabagini wilayani Meatu mkoani Simiyu kuhusu umuhimu wa sekta ya mafuta na gesi nchini



Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) lilishiriki katika Kongamano la 10 la Jotoardhi Barani Afrika (ARGeo-C10) na kutoa elimu katika sekta ya mafuta na gesi kwa Wadau mbalimbali, kongamano hilo lilifanyika katika Kituo cha mikutano cha Kimataifa cha Mwl. Julius Nyerere (JNICC) Oktoba, 2024 Jijini Dar es salaam





Tanzania Petroleum Development Corporation (TPDC)

EDITORIAL

Welcome to this special edition of the TPDC magazine, dedicated to providing you with insights into the implementation of the various responsibilities of the Organization. In this edition, you will learn about our successes, the challenges we face, and the continuous efforts we put forth to solve these challenges, ensuring that the nation benefits from our presence.

First and foremost, we are delighted to clarify the role and significance of TPDC in the country's economy. This magazine serves as an opportunity for you to better understand how TPDC contributes to the nation's growth, development, and prosperity. Through this publication, we aim to shed light on the work we do, the impact we make, and how we strive to improve the lives of the people we serve.

As a public organization, we are committed to responding to the needs of our stakeholders in accordance with the law. We uphold the principles outlined in the laws governing public organizations, including the Petroleum Act, 2015, which guides our operations. Our primary responsibility is to ensure that our activities generate profits, which contribute to the overall development of the nation and support the government's revenue generation.

At TPDC, we view ourselves as a crucial pillar of the nation's development. Through our efforts in oil and natural gas exploration, as well as the transportation and distribution of natural gas across the country, we have become a key energy provider. Our contribution is significant, as we are not only the main source of natural gas but also a vital provider of electricity, powering the country's growth and industrialization.

The Tanzania Petroleum Development Corporation (TPDC) has played a crucial role in driving the growth of the country's industrial sector since its establishment in 2015. By ensuring the reliable supply of natural gas energy, TPDC has positioned itself as a key enabler for large-scale investments across various industries in Tanzania. These industries are not only vital for the nation's economy but also serve as the main employers and significant contributors to the government revenue through taxes. Furthermore, industrial growth helps stimulate other vital sectors, including mining, agriculture, healthcare, and education.

With a firm belief that energy reliability is a fundamental pillar for investment, TPDC has diligently worked to ensure that Tanzania is equipped with sufficient, affordable, and dependable energy. This includes the development of natural gas processing infrastructure in key locations such as Madimba in Mtwara and Songo Songo in Lindi. In addition to this, the corporation has invested in a robust pipeline system capable of transporting large quantities of natural gas.

Moving forward, TPDC is focused on expanding its capacity to meet both domestic and international energy needs, through projects aimed at increasing natural gas availability. By doing so, TPDC continues to contribute significantly to Tanzania's economic development and positions the country as an attractive destination for both local and foreign investors.

Mussa Makame, the Executive Director of the Tanzania Petroleum Development Corporation (TPDC), has provided an update on the organization's efforts to increase the country's natural gas production and its role in the oil and gas sector. Currently, TPDC is collaborating with investors, including ARA Petroleum and Ndovu Resources, to significantly boost the natural gas supply from the Ntorya field. Starting with an increase from 60 million cubic feet to 140 million cubic feet within three years, the project will also see the installation of plants designed to enhance production capacity at the Mnazi Bay block wells. In this area, production is expected to rise by an additional 20 million cubic feet.

Additionally, TPDC is working with M&P to drill two new wells in the Mnazi Bay block, which is part of ongoing efforts to ensure the nation has sufficient gas supply. These developments are part of a broader strategy that also includes conducting research in other regions and forging new investment agreements in Tanzania's oil and gas sector.

Makame emphasized TPDC's commitment to the nation, stating that the corporation has a crucial role in safeguarding the country's interests in the sector, as well as holding shares in development blocks and operations. He noted that the recent agreements, including TPDC's purchase of a 60-billion-shillings share in the Mnazi Bay block, represent a significant milestone both for the organization and for the country.

